



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO  
**BODI YA FILAMU TANZANIA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**Dar es Salaam - 19 Machi, 2021**

Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Tanzania inawaelekeza wadau wote wanaojihusisha na shughuli za Filamu na Michezo ya Kuigiza kwa Tanzania Bara kusitisha Matamasha yote yanayohusiana na filamu na michezo ya kuigiza na/au uzinduzi wa filamu utakaoambatana na sherehe, isipokuwa filamu na michezo ya kuigiza yenye maudhui yanayolenga maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwa muda wa siku 21, kuanzia tarehe 17 Machi, 2021 mpaka tarehe 8 Aprili, 2021.

Sitisho hili linafuatia tangazo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan la maombolezo ya siku 21, alilolitoa tarehe 19 Machi, 2021.

Aidha, kwa maelezo zaidi kuhusiana na sitisho hili, wasiliana na Bodi ya Filamu Tanzania kwa namba; +255 22 2121920 / 0712683271.

Imetolewa na:

Dkt. Kiagho Kilonzo

**Katibu Mtendaji,**

**Bodi ya Filamu Tanzania.**